HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHE. ENG. EVARIST NDIKILO, KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA CHAURU (CHAURU DAY) TAREHE 10 OKTOBA, 2020 WILAYANI BAGAMOYO

- ***Mhe Zainabu Kawawa, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo,***
- ***Mwakilishi wa Mrajis na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Nchini,***
- ***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze,***
- ***Wataalam ngazi ya Mkoa na Halmashauri,***
- ***Mwenyekiti wa Bodi na Menejimenti ya CHAURU,***
- ***Wawakilishi kutoka TADB, NHIF, AGRITERA na AGRICOM,***
- ***Wanachama wa Ushirika Umwagiliaji Ruvu- CHAURU,***
- ***Wadau wa Maendeleo ya Ushirika***
- ***Wageni waalikwa,***
- ***Wanahabari,***
- **Mabibi na Mabwana**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana kwa ajili ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU DAY).

Pili, niwashukuru Viongozi na Wanachama wa CHAURU kwa kunipa heshima na kunialika mimi na wenzangu ili tuweze kushiriki kwenye siku hii muhimu. Nasema asanteni sana kwa kututhamini.

Tatu, napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa maandalizi mazuri ya siku yenu. Nimebahatika kutembelea maeneo mbalimbali ya shughuli zenu. Kwa kweli maandalizi ni mazuri sana. Hongereni sana CHAURU kwa maandalizi haya.

Ndugu Wana- CHAURU;

Kuamua kuwa na siku hii (Siku ya CHAURU) ni ishara kuwa mnatambua kwa dhati umuhimu wa Umoja miongoni mwenu. Ni Siku inayowaunganisha Wanaushirika wote wa CHAURU na Wadau wengine wa Maendeleo ya Ushirika ili kwa pamoja muweze kutafakari na kujitathmini mlipotoka, mlipo na mnapoelekea na hatimaye kuweka mikakati ya namna ya kusonga mbele katika shughuli zenu za kujikwamua kiuchumi.

Ubunifu huu ni jambo jema na unastahili kupongezwa na kila mmoja wetu. Hongereni sana Wana- CHAURU

Ndugu Wana- CHAURU;

Wakati ninatembelea maeneo mbalimbali ya Ushirika wenu, nimeona fursa nyingi. Licha ya shughuli mama ya shamba lenu ya

kilimo na ukoboaji wa mpunga, nimeshuhudia pia kilimo cha korosho kwenye mashamba ya malimbichi ambapo baadhi ya wakulima wamepanda mikorosho na ninasikia wengine wameanza kuvuna sasa. Nawapongeza sana Bodi na Menejimenti ya CHAURU kwa kutekeleza agizo langu la mwaka jana la kupanda mikorosho. Nimeambiwa pia kuna fursa za kilimo cha mbogambaga na matunda kwenye eneo la bonde lenye hekta 1,500 ambazo pia zinafaa kwa ufugaji wa samaki, fursa za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa nk. Nichukue fursa hii kuwapa rai wana-CHAURU kuendelea kuzitumia fursa zote zinazopatikana hapa ili kujiongezea vipato na kuondokana na utegemezi kwenye mpunga kama zao pekee.

Niwaagize tena viongozi wa CHAURU kuhakikisha mnasimamia na kuwahamasisha wanachama wenu kutumia fursa zinazopatikana ipasavyo ili waondokane na umasikini wa kipato na kujitosheleza kwa chakula.

Ndugu Wana-CHAURU,

Sote tunafahamu azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukuza uchumi wa wananchi na kuondokana na umaskini kupitia ujenzi wa viwanda. Kupitia azma hiyo, nchi yetu sasa imefanikiwa kuwa Nchi yenye Uchumi wa Kati na inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuanzisha na kuendeleza viwanda. Sekta ya Ushirika

inaweza kutoa mchango mkubwa katika kuwezesha kutimia kwa azma hiyo ya Serikali. Wakati ninakagua maeneo mbalimbali nimetembelea mashine yenu ya kukoboa mpunga. Hakika nimefarijika sana kwa hatua mliyofikia. Nitumie fursa hii kuwapa rai ya kuongeza mashine za kufungasha mchele wenu ili muweze kuuza bidhaa iliyo bora kutoka CHAURU.

Ndugu Wana-CHAURU;

Risala yenu imetaja changamoto mbalimbali, ikiwemo Uchakuvu wa Miundombinu ya Umwagiliaji, Ubovu wa barabara, Uvamizi wa mifugo na Malalamiko ya baadhi ya wananchi kutoka kwenye Vijiji vinavyozunguka eneo la ushirika ya kutengwa na ushirika huu.

Kuhusiana na uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji, mtakumbuka kwenye maadhimisho yaliyopita Benki ya kilimo walionesha nia ya kutoa mkopo ili muweze kukarabati miundombinu ya shamba ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo chenu. Nitumie fursa hii kwa mara nyingine kuwakumbusha Benki ya Kilimo, na kwa bahati nzuri wapo hapa watoe mkopo huo ili ukarabati ufanyike na changamoto hii iishe kabisa.

Kuhusu ubovu wa barabara kutoka makutano ya lami na barabara inayokuja shambani, naagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze ukae na TARURA Wilaya ili kuona namna ya kuikarabati

barabara hii kutokana na ukweli kwamba eneo hili ni la kiuchumi na Halmashauri inapata mapato makubwa kutoka eneo hili.

Suala la mifugo limeendelea kuwa changamoto kubwa. Ningependa kutoa rai kwa wafugaji kuheshimu maeneo ya kilimo sawa na jinsi wakulima wanavyopaswa kuheshimu maeneo ya wafugaji. Kwa eneo la CHAURU lenye mifereji iliyosakafiwa, kuingiza mifugo ni hatari zaidi kwa sababu kwato za mifugo zinavunja mifereji hiyo na kuathiri umwagiliaji. Uongozi wa Wilaya na Halmashauri, Tarafa, Kata na Vijiji vinavyozunguka eneo hili mnapaswa kusimamia taratibu za kilimo na ulishaji wa mifugo. Kunapotokea migogoro hakikisheni inatatuliwa kwa haki. Nimeambiwa kuna matumizi makubwa ya rushwa ili kunyamazia kero za makundi yanayoonewa. Naagiza Mkuu wa Wilaya ulifanyie kazi suala hili. Taasisi zote zinazohusika na usimamizi na utatuzi wa migogoro zizingatie miiko na maadili ya kazi zao. Na ningependa kupata taarifa ya utekelezaji wa suala hili na mikakati itakayokuwa imewekwa baada ya mwezi mmoja kuanzia leo.

Kuhusu malalamiko; Nimefuatilia sana malalamiko ya wananchi wanaozunguka eneo hili kutengwa na ushirika huu na kubaini kwamba ushirika upo wazi kwa watu wote. Napenda kuwahimiza wananchi wanaopenda kujiunga na Ushirika wa CHAURU kufanya hivyo. Viongozi wa Vijiji na Vitongoji tuwahamasishe

wananchi wanaopenda kujiunga wajiunge. Hata hivyo wanatakiwa kuelimishwa kwamba kujiunga kwenye ushirika kuna taratibu zake ambazo pia zinaambatana na malipo fulani Fulani kama viingilio, hisa nk. Niwasihi viongozi muendelee kuwaelimisha wananchi wenu kuhusu taratibu hizo. Aidha, wakaribisheni Wataalam wa CHAURU kwenye Mikutano Mikuu ya Vijiji ili watoe elimu hiyo mbele ya wananchi. Bilas haka hii inaweza kupunguza au kuondoa kabisa malalamiko ya aina hiyo.

Ndugu Wana-CHAURU;

Mwisho, nirudie tena kuwashukuru wote kwa maandalizi na kushiriki siku hii ya maadhimisho ya Siku ya CHAURU. Niwatakie kila la heri katika sughuli zenu za kila siku. Niwaombe muendelee kudumisha umoja miongoni mwenu ili CHAURU iendelee zaidi. Wale wote wenye majukumu maalumu ya kutatua changamoto wafanye hivyo ili tutakapokutana tena mwakani kusiwe tena na changamoto hizo.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Siku ya CHAURU, yaani CHAURU DAY imefikia Kilele chake.

“Ushirika Pamoja Tujenge Uchumi”

Asanteni kwa kunisikiliza